



## **BENKI KUU YA TANZANIA**

### **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

#### **TOLEO JIPYA LA NOTI**

#### **SHILINGI ELFU MBILI (2,000)**

Mojawapo ya majukumu makubwa ya Benki Kuu ya Tanzania ni kutoa noti na sarafu za taifa la Tanzania.

Benki Kuu ya Tanzania mwaka huu wa 2009 imetoa noti za shilingi 2000 zenye saini tofauti na zile ambazo zimekuwepo katika mzunguko. Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania ameridhia utoaji wa noti hizi ili kukidhi mahitaji ya noti hizo katika mzunguko. Noti hizo mpya, zina tofauti moja tu na zile ambazo zimeendelea kuzunguka sasa, nayo ni **saini** zilizopo katika noti hizo. **Saini** zilizomo katika noti hizi mpya ni zile za Waziri wa Fedha na Uchumi; Mhe. Mustafa Mkulo (Mbunge), na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; Prof. Benno J. Ndulu; ambao kwa sasa, wapo **madarakani**.

Noti hizo bado zina rangi tawala ya kahawia. Aidha zina michoro inayoonesha mandhari ya Kitanzania ya kiuchumi, kiutamaduni, pamoja na urithi wetu na mazingira, kama ifuatavyo:

Mbele ya noti, bado kuna picha tawala inayoonesha utajiri wetu wa kuwa na mojawapo ya wanyama pori wakubwa; yaani Simba; alama ya kificho ya Twiga; ambayo bado ipo kama ilivyo katika noti nyingine zinazozunguka sasa.

Nyuma ya noti, bado kuna picha tawala inayoonesha picha ya Ngome Kongwe iliyopo Forodhani, katika Jiji la Zanzibar; picha ya kinyago cha kuchonga na alama ya usalama inayobadilika rangi ikigeuzwa geuzwa.

Wananchi wanashauriwa kuwa hakuna haja ya kubadilisha noti za sasa za TZS 2000 kwa noti hizi mpya, kwani thamani ni ileile, na hizi zinazozunguka sasa hazijafutwa katika mzunguko wa pesa.

Ni matumaini ya Benki Kuu ya Tanzania kuwa wananchi wataendelea kuwa makini kuchunguza na kutambua alama zilizopo katika noti zetu zote ili kuepuka kulaghaiwa na wahalifu.

*(Imesainiwa)*

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Agosti 2009**